

KUTHIBITISHWA KAZINI

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Ndugu msomaji wiki iliyopita tuliangalia umuhimu wa kusajili walimu katika Utumishi wa Umma. Leo tutaendelea kuelezea uthibishwaji kazini kwa walimu kama sehemu ya ufafanuzi juu ya mswali yaliyolizwa na baadhi ya wasomaji wetu. Ajira ya mwalimu haikamiliki hadi awe amethibitishwa kazini. Mara mwalimu anapoajiriwa hujaza mkataba na mwajiri wake na kwenye mkataba ameelezwa wazi kuwa atakuwa katika kipindi cha majaribio (probation period) kisichozidi miezi 12. madhumuni ya kipindi cha majaribio ni kutoa nafasi ya kutathmini uwezo wa mwalimu wa kufanya kazi na kama anastahili kuajiriwa katika utumishi wa umma. Mwisho wa kipindi cha majaribio, mwalimu anayeonyesha kumudu vizuri majukumu yake atapewa barua ya kuthibitishwa kazini.

1.0 JE, MWALIMU HUTHIBITISHWA KAZINI NA NANI?

Tofauti na makundi mengine ya watumishi wa umma ambayo mwajiri na mamlaka ya ajira ni huyo huyo, kwa walimu waajiri wao ni wengi na mamlaka yao ya ajira na nidhamu ni Idara ya Utumishi wa Walimu(TSD). TSD ndiyo humthibitisha kazini mwalimu. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002 kifungu 6(4) na Kanuni Na. 6(h) ya kanuni za Utumishi wa Umma, 2003.

2.0 JE, NI UTARATIBU GANI HUTUMIKA ILI MWALIMU AWEZE KUTHIBITISHWA KAZINI?

Ili mwalimu aweze kuthibitishwa kazini zipo hatua kadhaa za kufuata. Hatua ya kwanza ni msimamizi au mwajiri wa mwalimu kutoa taarifa ya utendaji kazi wa mwalimu kwa mamlaka ya ajira (TSD) miezi mitatu kabla ya kipindi cha majaribio kwisha. Katibu TSD wilaya atawasilisha mapendekezo ya walimu kuthibitishwa kazini kwa kamati ya wilaya ambayo nayo hutoa maoni yake kwa kamati ya mkoa (TSD). Kamati ya mkoa hutoa maamuzi na Katibu TSD mkoa huwaandikia barua za kuthibitishwa kazini walimu wote waliokubaliwa.

Mwalimu hataweza kuthibitishwa kazini iwapo atashindwa kudhihirisha kuwa anamudu majukumu ya ajira yake katika muda wa majaribio. Mwalimu anaweza kuongezewa muda wa kipindi cha majaribio mara moja tu kwa muda usiozidi nusu ya kipindi cha majaribio cha mwanzo mradi tu kuwe na matumaini ya kuboresha utendaji. Iwapo mwalimu atashindwa kudhihirisha kumudu majukumu yake ataondolewa kazini.

3.0 JE NI LAZIMA WALIMU WOTE KUWA NA BARUA ZA KUTHIBITISHWA KAZINI?

Walimu wote walioanza kazi tarehe 1.1.1988 na baada ya hapo ni lazima kuwa na barua za kuthibitishwa kazini. Walimu walioanza kazi kabla ya tarehe 1.1.1988 si lazima wawe na barua za kuthibishwa kazini kwa kuwa kanuni Na 58 ya zilizokuwa kanuni za TSC, 1990 ziliwasamehe kuwa na barua hizo.

4.0 NINI FAIDA AU MADHARA YA KUTOTHIBITISHWA KAZINI?

Kuthibitishwa kazini ni haki ya mwalimu. Mwalimu aliyethibitishwa kazini anajiamini zaidi, ana haki ya kupandishwa vyeo au kupewa madaraka mengine kazini. Wakati wa kustaafu kwa hiari, lazima au ugonjwa, mwalimu atalazimika kutoa barua ya kuthibitishwa kazini ili aandaliwe mafao yake ya kustaafu. Hata inapotokea bahati mbaya mwalimu amefariki, barua ya kuthibitishwa kazini ni moja ya vielelezo muhimu katika kuandaa mirathi. Mwalimu asiye na barua ya kuthibitishwe kazini atakosa haki zake za kiutumishi na kusumbuka pasipo sababu.

5.0 CHANGAMOTO:

Idara ya Utumishi wa walimu katika kushughulikia suala la

kuthibitisha walimu kazini imekumbana na changamoto zifuatazo:-

- (i) Baadhi ya walimu kutokuthibitishwa kazini kwa muda mrefu na kutokujua umuhimu wake.
- (ii) Baadhi ya waajiri kushindwa kuwasilisha kwenye mamlaka ya ajira ya walimu utendaji kazi wa walimu wanaotakiwa kuthibitishwa kazini.
- (iii) Baadhi ya waajiri kutokujua/kutokuzingatia wajibu wao wa kuhakikisha kuwa walimu wao wanathibitishwa kazini.
- (iv) Walimu kutojua mamlaka inayowaandikia barua za kuthibitishwa kazini.

6.0 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO:

- (i) Waajiri wahakikishe kuwa walimu walio chini yao wamethibitishwa kazini kwa mujibu wa kanuni Na.14 ya kanuni za Utumishi wa Umma.
- (ii) Waajiri watoe taarifa za utendaji kazi za walimu na kwa wakati kwa mamlaka yao ya ajira.
- (iii) Makatibu TSD Mkoa na Wilaya wahakikishe kuwa kuthibitisha kazini walimu ni zoezi/ajenda ya kudumu katika vikao vyao.
- (iv) Kila mwalimu ahakikishe ana barua ya kuthibitishwa kazini isipokuwa wale walioanza kabla ya tarehe 1.1.1988 ambao wamesamehewa na kanuni 58 ya kanuni za TSC, 1990.

Ikiwa una maoni, ushauri au maswali tafadhali tuandikie:-

Katiibu,

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,

S.L.P. 9143,

Dar es Salaam.